

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA KUMI NA TANO**

**KIKAO CHA AROBAINI**

**04 JUNI, 2024**



## **ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

### **MKUTANO WA KUMI NA TANO**

**KIKAO CHA AROBAINI TAREHE 04 JUNI, 2024**

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**WAZIRI WA FEDHA:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

### **III. MASWALI:**

#### **OFISI YA RAIS (TAMISEMI):**

**516. MHESHIMIWA NEEMA GERALD MWANDABILA  
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Kituo cha Afya Mkulwe kitaanza kazi rasmi.

**517. MHESHIMIWA OMARI MOHAMED KIGUA  
(KILINDI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Zahanati ya Kijiji cha Masagalu - Kilindi.

**518. MHESHIMIWA ALLY MOHAMED KASSINGE  
(KILWA KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itawalipa Walimu Wastaafu wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa malipo ya *Arrears* na fedha za kusafirisha mizigo.

**519. MHESHIMIWA ABDALLAH JAFARI  
CHAUREMBO (MBAGALA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Barabara zipi zimetengewa fedha katika Mradi wa DMDP awamu ya kwanza na barabara zipi zipo DMDP awamu ya pili katika Jimbo la Mbagala.

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

**520. MHESHIMIWA ALEKSIA ASIA KAMGUNA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, lini Serikali itajenga fensi ya umeme Hifadhi ya Mikumi ili kuepusha usumbufu wanaopata Wananchi wanaopakana na Hifadhi hiyo.

**WIZARA YA UCHUKUZI:**

**521. MHESHIMIWA JOSEPH ZACHARIUS KAMONGA (LUDEWA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, lini Serikali itajenga Gati, Ghala na Jengo la Abiria katika Bandari ya Manda.

**522. MHESHIMIWA MWATUM DAU HAJI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:-

Je, nini sababu ya ongezeko la mara kwa mara la nauli za usafiri wa ndege nchini.

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

**523. MHESHIMIWA TUMAINI BRYCESON MAGESSA (BUSANDA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, lini Serikali itajenga VETA kwa kuzingatia wingi wa Watu kwenye Majimbo bila kujali ni Wilaya au Mkoa.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**524. MHESHIMIWA KILUMBE SHABANI NG'ENDA (KIGOMA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, nini mpango wa Serikali kudhibiti Wahamiaji haramu mipakani kabla hawajaingia nchini.

## **WIZARA YA MADINI:**

### **525. MHESHIMIWA DKT. PIUS STEPHEN CHAYA (MANYONI MASHARIKI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Madini:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwekeza kwenye Madini ya Chumvi na Magadi katika Kata za Majiri na Sanza Wilaya ya Manyoni.

### **526. MHESHIMIWA SYLVIA FRANCIS SIGULA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Madini:-

Je, Serikali imetoa motisha kiasi gani kwa Wanawake 300 walioahidiwa kununuliwa Leseni za Uchimbaji Madini na Mheshimiwa Rais.

## **WIZARA YA MAJI:**

### **527. MHESHIMIWA TIMOTHEO PAUL MNZAVA (KOROGWE VIJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, lini Serikali itakarabati Bwawa la Mayuyu ambalo ni muhimu kwa upatikanaji wa Maji kwa Wananchi wa Kata za Kerenge, Magoma na Makumba.

## **WIZARA YA KILIMO:**

### **528. MHESHIMIWA INNOCENT SEBBA BILAKWATE (KYERWA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Masoko ya Mazao ya Kimataifa ambayo yametelekezwa miaka mingi.

## **WIZARA YA FEDHA:**

### **529. MHESHIMIWA STELLA IKUPA ALEX (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:-

Je, Serikali imekamilisha kuchakata na kufahamu idadi ya Watu wenye Ulemavu kwa kila Halmashauri kwa mujibu wa Sensa ya Mwaka 2022.

## **IV. HOJA ZA SERIKALI:**

### **WAZIRI WA FEDHA:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025.

**DODOMA  
04 JUNI, 2024**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*  
KATIBU WA BUNGE**